Mafunzo kwa Kamati ya Kitaalamu ya Wilaya (DDTC)

# Muhtasari kuhusu udhibiti wa Dawa

imetayarishwa na TFDA/MSH

# Malengo ya Mafunzo

Mwisho wa mafunzo washiriki wataweza:

- Kuelezea mfumo wa udhibiti wa dawa nchini
- Kutaja vigezo vya kufungua maduka ya dawa muhimu
- Kuelezea taratibu za maombi duka la dawa muhimu
- Kuelezea jinsi maduka ya dawa muhimu yanavyopaswa kuendeshwa
- Kuelezea taratibu za ukaguzi wa maduka ya dawa

# Kwa nini kudhibiti dawa

- Kulinda afya za watumiaji wa dawa kwa kuhakikisha wanapata dawa zilizo bora, salama na fanisi

- Kuhakikisha biashara za dawa zinafanyika kwa kufuata sheria na taratibu

# Mamlaka ya Chakula na Dawa

- Mamlaka ya chakula na Dawa (Tanzania Food and Drugs Authority- **TFDA**) ilianzishwa chini ya sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi ya 2003
- Ni taasisi iliyo chini ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii
- Iliundwa kwa kuunganisha taasisi mbili (1) Bodi ya Madawa (ii) TUKUTA

# Ngazi za Udhibiti

- **Taifa** – Mamlaka ya Chakula na Dawa
- **Mkoa**- Kamati ya kitaalamu ya Dawa ya Mkoa (RDTC)
- **Wilaya** – Kamati ya Kitaalamu ya Dawa ya Wilaya (DDTC)
- **Kata** – Kamati Ndogo ya Afya ya Kata

# Majukumu ya TFDA

- Kuweka na kusimamia viwango vya ubora na usalama wa chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba
- Kudhibiti utengenezaji, uingizaji nchini, usambazaji na utangazaji wa chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba
- Kutoa vibali vya kuendesha biashara za bidhaa zinazodhibitiwa
- Kusajili bidhaa kabla ya kuruhusiwa kuingizwa katika soko

# Majukumu ya TFDA …….

- Kukagua sehemu zote zinazojihusisha na biashara ya vyakula, dawa na vipodozi
- Kufanya uchunguzi wa kimaabara ili kuthibitisha ubora na usalama wa bidhaa zinazodhibitiwa
- Kuboresha/kuchochea matumizi sahihi ya dawa (promote rational drugs use)
- *TFDA hushirikiana na Serikali za mikoa na Wilaya katika utekelezaji wa majukumu haya na taratibu zinafanyika ili baadhi ya majukumu yaweze kukasimiwa TAMISEMI*

# Kamati ya Kitaalamu ya Dawa ya Mkoa

- Imeundwa chini ya kanuni Na. 9 ya Kanuni za Maduka ya Dawa Muhimu
- Ina wajumbe 5:
  - Mkuu wa Mkoa
  - Mfamasia wa Mkoa
  - Mganga Mkuu wa Mkoa
  - Afisa Mifugo
  - Afisa Kilimo
  - Afisa Biashara

# Kamati ya Kitaalamu ya Dawa ya Wilaya ……

- Imeundwa chini ya vifungu 6,7 na 8 vya Kanuni za Maduka ya Dawa Muhimu
- Wajumbe:
- Mkuu wa Wilaya – M/Kiti
- DED - Makamu M/Kiti
- Mfamasia - Katibu
- Katibu Tawala (W)
- Mganga Mkuu (W)
- Afisa Biashara (W)

# Kamati ya Kitaalamu  ya Dawa ya Wilaya

- Afisa Afya
- Afisa Kilimo/Mifugo
- Mwanasheria wa Halmashauri ya Wilaya
- Mwakilishi wa jamii
- Mwakilishi wa NGO

# Kamati Ndogo ya Afya ya Kata

- Imeundwa chini ya kifungu Na. 39
- Wajumbe:
  - Mtendaji wa kata (WEO)
  - Mganga wa kituo cha afya kilicho katika kata
  - Afisa ugani (Extension Officer)
  - Afisa Afya
  - Afisa Maendeleo